

**HOTUBA YA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA  
LA MAPINDUZI, MHE. AL HAJJ DK. ALI MOHAMED SHEIN,  
KATIKA BARAZA LA IDD EL FITRI  
JULAI, 2016 (1 SHAWWAL, 1437)**

**BISMILLAH RAHMANI RAHIM**

Shukurani zote anastahiki Mola wetu Mtukufu Subhana Wataala; Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo ndani yake. Tunakiri kwa moyo na kutamka kwa ulimi kuwa Yeye peke yake ndiye anayestahiki kuabudiwa kwa haki. Na kwake Yeye ndiyo marejeo yetu sote. Tumuombe Mwenyezi Mungu atupe khatma njema katika marejeo yetu.

Sala na salamu zimshukie Mtume wetu Muhammad (S.A.W), Aali zake, Sahaba zake na waumini wote waliofuata njia yake ya uongofu. Inshaallah na sisi tuwe miongoni mwao. Tunamuomba Mola wetu (SW) atuwezeshe kuyatekeleza maamrisho yake na kujiepusha na makatazo yake ili tuweze kufanikiwa hapa duniani na huko akhera twendako.

**Mheshimiwa Samia Suluhi Hassan,  
Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,**

**Mheshimiwa Sheikh Saleh Omar Kabi;  
Mufti wa Zanzibar,**

**Mheshimiwa Dk. Amani Abeid Karume;  
Rais Mstaafu wa Zanzibar,**

**Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid;  
Spika wa Baraza la Wawakilishi,**

**Mheshimiwa Omar Othman Makungu;  
Jaji Mkuu wa Zanzibar,**

**Mheshimiwa Sheikh Khamis Haji Khamis;  
Kadhi Mkuu wa Zanzibar,**

**Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri,**

**Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi,**

**Viongozi mbali mbali wa Serikali,**

**Waheshimiwa Mabalozi,**

**Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

**Wageni Waalikwa,**

**Ndugu Wananchi,**

**Mabibi na Mabwana,**

**Assalamu Aleikum Warahmatullahi Wabarakatu**

**IDDI MUBARAK!**

Kwa hakika tuna wajibu mkubwa wa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuikamilisha funga ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa salama. Kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu ametuwezesha kufikia siku hii ya sikukuu tukiwa hai. Tukumbuke kwamba, walikuwepo waislamu wenzetu tulioanza kufunga nao, lakini kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu wametangulia mbele ya haki. Tumuombe Mola wetu awape malazi mema peponi na sisi azikubali ibada zetu zote tulizozifanya na atupe malipo mema.

## **Ndugu Wananchi,**

Leo ni siku ya sikukuu ya Idd el Fitri, ambapo waislamu wa Zanzibar na wananchi wote tunaungana na wenzetu katika mataifa mbali mbali katika kuisherehekea sikukuu hii muhimu ya furaha ikiwa ni mionganini mwa sikukuu adhimu alizotuvekeea Mwenyezi Mungu kwa kila mwaka. Imepokelewa kutoka kwa Imam Ahmad, Hakim, Abu Daud na An-nisai kwamba Bwana Mtume (S.A.W) alipohamia Madina na kuwakuta wakaazi wake wakisherehekea sikukuu kinyume na twaa ya Mwenyezi Mungu aliwaambia:

**"Hakika Mwenyezi Mungu amekubadilishieni sikukuu mbili, bora kuliko zenu mlizokuwa mkizisherehekea. Sikukuu ya Idd el Fitri na Idd el Hajj."**

Kwa hivyo, tuna wajibu wa kumshukuru Mola wetu kwa kutuwezesha kuifikia siku hii ya Idd el Fitri, tukiwa hai na wazima wa afya. Tumshukuru Mola wetu kwa kutujaaliya kusali sala za Idd katika maeneo mbali mbali kwa salama. Ni vyema tuendelee kuisherehekea siku hii kwa kufanya mambo yote ya halali pamoja na kuwatemebelea ndugu, jamaa na wagonjwa wetu walioko majumbani na hospitali na kuwaombea dua.

## **Ndugu Wananchi,**

Natoa salamu zangu za Idd kwenu nyote mliohuduria katika Baraza hili la Idd, kwa waislamu wote na kwa wananchi wote wa Zanzibar na

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yote kwa jumla. Nakutakieni nyote na familia zenu sikukuu njema, yenye kheri na baraka nyingi. Kwa baraka za siku hii, tumuombe Mola wetu aizidishie nchi yetu amani na mshikamano ili iwe sababu ya kupiga hatua zaidi za maendeleo na ustawi wa jamii yetu.

Hatuna budi tumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba waislamu katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu, leo asubuhi tumejitokeza kwa wingi kusali sala ya Idd na sisi kwa niaba ya wenzetu, tumekusanyika hapa kuhudhuria katika Baraza hili la Idd katika hali ya amani na utulivu. Hiki ni kielelezo chema cha mshikamano na umaja wetu katika kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Tumuombe Mola wetu azidi kuuimarisha umaja na mshikamano wetu na aupe baraka mkusanyiko wetu huu.

### **Ndugu Wananchi,**

Jana tumeukamilisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, mwezi ambao una utukufu mkubwa kwa waislamu. Huu ndio mwezi ulioteremshwa kitabu kitukufu cha Qurani ili uwe muongozo na uongofu kwetu sote. Mwenyezi Mungu ametubainishia katika aya ya 185 ya Suratul Bakarah yenye tafsiri isemayo:

***"Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa ndani yake  
Qurani kuwa ni uongofu kwa watu, na hoja zilizo wazi na  
uwongofu na upambanuzi, ....."***

Utukufu mwengine wa Mwezi wa Ramadhani ni kwamba, amali za waja katika kufanya ibada huwa na fadhila kubwa zaidi kuliko miezi mengine

ikiwa ni pamoja na kusamehewa makosa yote iwapo tulifunga kwa imani na kumtegemea Yeye Mwenyezi Mungu. Imepokelewa kutoka kwa Imaam Al-Bukhariy na Muslim, kwamba Mtume Muhammad (S.A.W) amesema:

***"Atakayefunga Ramadhani kwa imani na kutaraji malipo, ataghufiriwa madhambi yake yaliyotangulia"***

Katika hadithi nyengine mashuhuri, Mtume Muhammad (S.A.W) amesema:

***"Enyi watu! Hakika umewaelekeeni nyinyi Mwezi wa Ramadhani kwa baraka, rehema na msamaha, mwezi ambao ni bora mbele ya Mwenyezi Mungu kuliko miezi yote, siku zake ni bora kuliko siku zote, na saa yake ni bora na muhimu kuliko saa zote"***

Kwa mnasaba wa hadithi hiyo, ni dhahiri kuwa ibada zote tulizozifanya katika Mwezi wa Ramadhani zilikuwa na fadhila kubwa zaidi kuliko zile tunazozifanya katika miezi mengine. Tumuombe Mwenyezi Mungu atujaalie tuwe mionganini mwa walionufaika na fadhila kubwa za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani tulioukamilisha na aendelee kutudumisha katika ibada.

### **Ndugu Wananchi,**

Pamoja na fadhila tulizozipata katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kutokana na kuongeza jitihada zetu katika kufanya ibada mbali mbali,

zikiwemo kusali sala za jamaa na sunna, kusoma Qurani, kutoa sadaka na kujizuwia kufanya maovu mbali mbali, bila ya shaka Mwenyezi Mungu atatujaalia kupata faida nyengine muhimu iwapo tutaendelea na mwendo huo katika maisha yetu ya kila siku. Tuendelee na mafunzo tuliyoyapata katika kipindi cha mwezi mtukufu wa Ramadhani. Katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani tumepata mafunzo mengi muhimu, miongoni mwa mafunzo hayo tuliyoyapata ni kuwa na subira, ucha Mungu, kuhurumiana na kupendana.

Katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, tulijifunza kusubiri kwa kukaa kutwa bila ya kula, kunywa na kufanya mambo mengine ya halali ikiwa ni kubainisha utii wetu kwa Mwenyezi Mungu na kutegemea kupata malipo bora kama ilivyobainishwa katika hadithi ya Mtume Muhammad (S.A.W) aliposema:

***"Huu mwezi wa Ramadhani ni mwezi wa kusubiri na hakika subira malipo yake ni pepo"***

Vile vile, tulijifunza subira kwa kujizuwia kufanya vitendo viovu na badala yake tulijitahidi katika kufanya mambo mema. Tulijitahidi na tulidhamiria katika kutafuta riziki za halali, kuacha kusema uongo, kuacha kusengenya na vitendo vingine viovu. Jamii yetu ilijaa nuru ya mapenzi na imani, pamoja na watu kucaa mavazi ya heshima yenye kuzingatia mafundisho ya dini. Subira ilihuisha imani na utii wetu mbele ya Mola wetu. Funga zetu zilikuwa ni baina yetu na Mola wetu tukiwa na imani kwamba anatuona na anavijua vitendo vyetu vyote na Yeye ndiye atakae tulipa. Katika kipindi chote cha Ramadhani tulimuweka

Mola wetu mbele na kutegemea kupata rehema zake, maghfira na kutuepusha na moto.

Hatuna budi tuendelee na mwendo huu wa kuwa na subira tuliojifunza, kwani mwendo huu una faida kubwa kwa manufaa ya jamii yetu hapa duniani na kama alivyosema Mtume wetu Muhammad (SAW), malipo yake ni pepo. Tumuombe Mwenyezi Mungu atupe uwezo katika hayo.

### **Ndugu Wananchi,**

Ucha Mungu ni miongoni mwa ya mafunzo muhimu yanayotokana na Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Maulamaa wengi wamekubaliana kuwa ucha Mungu ni kujitenga katika kufanya madhambi na kila alichokiharamisha Mwenyezi Mungu na kutekeleza maamrisho yake. Sote tulijitahidi na tulidhamiria tuwe na mwendo mwema katika kipindi chote cha saumu. Hata hivyo, ni vyema tukatanabahi kuwa mwendo na wajibu wetu huo tunapaswa uwe wa kudumu na sio uwepo katika kipindi cha mwezi wa Ramadhani peke yake.

Katika aya ya 10 ya Surat Azzumar, Mwenyezi Mungu anamwambia Mtume wetu Muhammad (S.A.W) atwambie sisi wafiasi wake kuhusu ucha Mungu na kuwa na subira katika tafsiri isemayo:

***"Sema: Enyi waja wangu mliaoamini! Mcheni Mola wenu mlezi. Wale wafanyao wema katika dunia hii watapata wema. Na ardhi ya Mwenyezi Mungu ni kunjufu. Hakika wenye subira watapewa ujira wao bila ya hisabu."***

Aya hii ya Mwenyezi Mungu inatupa habari njema iwapo tutaendelea na ucha Mungu pamoja na kusubiri na kwamba faida yake ni kupata mafanikio na radhi za Mwenyezi Mungu bila ya kiwango. Tumuombe Mola wetu atujaalie tuwe nao mwendo huo na kamwe tusiuwache.

### **Ndugu Wananchi,**

Sote tumeshuhudia kwamba ushirikiano wetu, mapenzi baina yetu na kusaidiana kuliongezeka katika kipindi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Kama sote tujuavyo, hatukuweza kuendeleza utamaduni wetu wa kufutari pamoja na kupelekeana vyakula vya tunu kutokana na mtihani wa maradhi ya kipindupindu. Hata hivyo, tulienendeza ushirikiano wetu kwa kuwa pamoja katika sala za jamaa na darsa misikitini na katika vikao vya itikafu na mashindano ya Quran yaliyoandaliwa katika mwezi wa Ramadhani.

Napenda nitumie fursa hii, kutoa shukurani zangu za dhati kwa Masheikh na Walimu wetu waliofanya kazi kubwa ya katika darsa mbali mbali na kutukumbusha juu ya maamrisho ya Mwenyezi Mungu pamoja na nasaha walizotupa ili tuweze kufanikiwa hapa duniani na kesho akhera. Tumuombe Mola wetu awajaalie kila la kheri na mafanikio mema na sisi atujaalie tuyajendeleze tulijojifunza.

Ni dhahiri kuwa mambo mema yote tuliyotendeana bado yanahitajika kuelezw na kutekelezwa wakati wote hata baada ya kumalizika kwa mwezi wa Ramadhani. Tuuendeleze mwendo huu mwema huku tukizingatia kuwa sote ni wamoja na tunamtegemea Mwenyezi Mungu mmoja (S.W).

## **Ndugu Wananchi,**

Natoa wito kwa viongozi wote wa vyama vyaa siasa tuzingatie kuwa ni jukumu letu sote, kuhimiza utiifu wa sheria zetu, amani, utulivu na usalama wa nchi yetu na tuhurumiane na tupendane. Kwa hivyo, sote ni wamoja na tuna jukumu la kuishi kwa amani, umoja, mshikamano na kupendana. Lazima tutimize wajibu wetu huo kwa sababu Zanzibar ni nchi yetu sote na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi yetu sote.

Viongozi hatupaswi kuwachochea wafuasi wa vyama vyetu wafanye fujo, wahasimiane, wanuniane, wagomeane kwenye huduma za jamii na dini, wabaguane na zaidi ya hayo wasielekezwe kufanya vitendo vyaa hujuma ndani ya jamii yao.

Viongozi wa siasa wanaowachochea wafuasi wao kufanya vitendo vyaa ubaguzi, hujuma na ujisadi wa kuyaharibu mazao, miti na mimea ya chakula na biashara pamoja na kuifanya ukatili mifugo ni kinyume cha maamrisha ya Mwenyezi Mungu. Matokeo ya vitendo hivyo, ni kuzikufuru neema za Mwenyezi Mungu alizotuletea. Baadhi ya vitendo hivi viovu vilifanywa hivi karibuni huko Pemba kabla ya mwezi wa Ramadhani na ndani ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Vitendo hivi vimeitia aibu nchi yetu na si sehemu ya mafunzo tuliyoyapata katika Ramadhani ya mwaka huu na zilizopita na hayaendani na maadili ya dini na maamrisha ya Mwenyezi Mungu.

Napenda nikukumbusheni kwamba saumu hutujengea hisia za usawa za watu wenye hali na uwezo tafauti wa kipato mbele ya Mwenyezi Mungu. Mafunzo tunayoyapata katika saumu hayatufundishi kufanya ubaguzi, dharau, kejeli na kibri mionganini mwetu. Tunapaswa turudi kwa Mola wetu kwa kuyazingatia maamrisha yake. Ni vyema, kila mmoja wetu awe makini na watu ambao wanavuka mipaka na kudharau mafunzo ya dini, mila na tamaduni zetu.

### **Ndugu Wananchi,**

Kila mmoja wetu ajitahidi kuepuka vitendo viovu ambavyo huambatana na ushawishi wa Shetani. Mwenyezi Mungu ametubainishia, katika aya ya 21 ya Surat Nur, yenye tafsiri isemayo:

***"Enyi mlionamini! Msifuate nyayo za Shetani; na atakayefuata nyayo za Shetani (atapotea) kwani yeye huamrisha mambo ya aibu na maovu; na lau kuwa si fadhila za Mwenyezi Mungu na rehema yake juu yenu asingalitakasika mionganini mwenu hata mmoja, lakini Mwenyezi Mungu humtakasa amtakaye na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia na Mwenye kujua."***

Kadhalika, Mwenyezi Mungu anatukumbusha na anatuhimiza kwenye Qurani kwamba, tuzishukuru neema zake. Miti na mimea mengine ni ishara ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu na imeumbwa ili itupe wepesi katika maisha yetu. Tusivuke mipaka na kudharau neema hizi kwa kuikata miti, mimea ya chakula na kadhalika kwa kuwa tunatafautiana katika itikadi zetu za kisiasa.

Mwenyezi Mungu ametubainishia neema zake na umuhimu wa mimea kwetu katika aya 10 ya Surat Nahl , yenye tafsiri isemayo:

**"Yeye ndiye anayekuteremshieni maji kutoka mawinguni, kwa hayo mnapata kinywaji, na kwa hayo (inatoa) miti ambayo humo mnalisha (wanyama)"**

Na katika aya ya 11 ya Sura hiyo :

**"Na kwa hayo hukuotesheeni mimea (ya kila namna) na mizaituni na mitende na mizabibu na kila matunda. Na bila ya shaka ,katika hayo imo ishara kwa watu wenyewe kufikiri ( kuwa yuko Mwenyezi Mungu)."**

Ni wajibu wetu kuzishukuru neema tulizobarikiwa na Mweyezi Mungu kwa kuziheshimu, kuzitumia vizuri; badala ya kuonesha kibri, kuzidharau na kutozijali. Kwa kuzishukuru neema hizo, tutapata faida kubwa ya kupata chakula cha kutosha na mapato ya kujikimu katika maisha yetu ya kila siku.

### **Ndugu Wananchi,**

Nachukua fursa hii kutoa pole kwa wananchi wote walioharibiwa mali zao, mazao yao, mifugo yao na kupata usumbufu wa aina mbali mbali. Nawaomba waliofikwa na maafa haya wawe na subira na ustahamilivu. Serikali iko pamoja nao na tayari imeanza kuchukua hatua dhidi ya waliofanya vitendo hivyo.

### **Ndugu Wananchi,**

Tutumie mafunzo ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na mafundisho ya dini kwa kujiepusha na vitendo vya husda, kuchukiana na uhasama kwa visingizio mbali mbali. Vitendo vya aina hii havina faida na ni kichocheo kikubwa cha kuharibu amani na utulivu tulionao. Katika kutuasa na ubaya wa kuendeleza vitendo hivyo, katika hadithi iliyopokelewa na Imamu Bukhari na Muslim, Bwana Mtume Muhammad (S.A.W) amesema:

***"Msihusudiane, msichukiane, wala kuoneana. Na kuweni na umoja na mshikamano, mambo yatanyooka, amani kusambaa na maendeleo kustawi"***

Hadithi hii ina mnasaba na mazingira tunayopaswa kuwa nayo hasa wakati huu baada ya kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu wa tarehe 20 Machi, 2016 ambao matokeo yake yalitangazwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar tarehe 21 Machi, 2016 ambapo Chama cha Mapinduzi kilishinda kwa asilimia 91.4. Kwa hivyo, baada ya kufanyika uchaguzi huo, hakutokua na uchaguzi mwengine wowote utakaofanyika, hadi hapo mwaka 2020. Uchaguzi umekwisha. Serikali iliyochaguliwa na wananchi imekwishaundwa na ipo madarakani na imeanza kutekeleza majukumu yake. Kwa hivyo, kutokana na matokeo hayo ya uchaguzi, na kwa kuzingatia Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, hakuna Serikali ya mpito itakayoundwa hapa Zanzibar. Hayo yanayosemwa mitaani ni hadithi ya "Sadiki Ukipenda". Na upotoshwaji mkubwa unaofanywa na wapotoshaji. Wajibu wa wananchi ni kushirikiana na Serikali yao katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo yetu katika nyanja mbali mbali. Mipango yetu ya maendeleo na uwezekano wa kuyafikia malengo

tuliyojiwekea itatekelezeka vyema iwapo tutaongeza ushirikiano na kuishi kwa amani.

Serikali tayari ishaanza kuitekeleza Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya mwaka 2015/2020 lakini zinajitokeza ishara na vitendo vyta kutaka kutuchelewesha kuitekeleza Ilani yetu. Natoa indhari kwamba sitomvumilia mtu yoyote au kikundi chochote kitakachorajibu kutuchelewesha kwa mbinu yoyote ile; katika kuyatekeleza majukumu ya Serikali na kuitekeleza Ilani ya CCM. Watakaokuwa na nia hio hawatofanikiwa kwani watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

### **Ndugu Wananchi,**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba katika kipindi chake cha pili tayari imetangaza bajeti yake ya TZS bilioni 841.5 katika mwaka wa fedha 2016/2017 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Aidha, Wizara zote 13 zilizoundwa kusimamia sekta mbali mbali nazo ziliwasilisha bajeti zao katika vikao vyta Baraza la Wawakilishi vilivyoanza tarehe 18 Mei, 2016 na kumalizika tarehe 29 Juni, 2016. Kwa mnasaba huo, Serikali imepata idhini ya wananchi kupitia wawakilishi wao iweze kutekeleza mipango iliyojipangia ili kupiga hatua kubwa zaidi za maendeleo, kiuchumi na kuimarisha huduma za jamii.

Serikali imedhamiria kwa dhati kuimarisha uwezo wake wa kukusanya mapato ya ndani, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ili kuongeza uwezo wetu katika kujitegemea na hatimae tuweze kupunguza utegemezi wa misaada ya nje hatua kwa hatua kwa kadiri itakavyowezekana. Jambo hili litawezekana iwapo kila mmoja wetu

atawajibika ipasavyo katika kutekeleza majukumu yake. Napenda nitumie fursa hii ili nimpongeze Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid kwa kazi nzuri ya kuliongoza Baraza la Wawakilishi kwa mafanikio. Kadhalika, nampongeza Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi kwa kusimamia vyema na kwa ufanisi mkubwa shughuli za Serikali kwenye Baraza la Wawakilishi, hasa kwenye kipindi cha Bajeti. Vile vile, nawapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kutekeleza wajibu wao ipasavyo na kuipitisha Bajeti ya Serikali pamoja na Bajeti za Wizara mbali mbali. Kadhalika, natoa shukurani na kuwapongeza Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwa umahiri wao katika uwasilishaji wa hotuba za bajeti na kujibu hoja za wajumbe kwa umakini mkubwa. Vile vile, nawapongeza wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa umahiri wao wa kuuliza maswali na kutaka ufanuzi wa mambo kadhaa kwa uwazi, uhakika na bila ya hofu. Shughuli za Baraza zilifana sana na mambo yalinoga.

### **Ndugu Wananchi,**

Napenda nisisitize kwamba kufanikiwa kwa utekelezaji wa mipango ya Serikali, kunategemea sana kuendelea kuwepo kwa hali ya amani na utulivu nchini. Kwa mara nyengine, natoa wito kwa viongozi wa kisiasa, madhehebu ya dini, taasisi za kijamii, wazazi na walezi tuendelee kusisitiza juu ya umuhimu wa kuilinda, kuienzi na kuiendeleza amani tuliyonayo kwa manufaa yetu. Serikali zetu zote mbili; Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zitaendelea kuchukua hatua madhubuti katika kuhakikisha kwamba amani na usalama vinakuwepo nchini.

Nchi yetu inaongozwa kwa misingi ya sheria na kwa kuzingatia Katiba. Kwa hivyo, hakuna mtu au kikundi cha watu kitakachokuwa juu ya sheria. Ni wajibu wa kila mmoja wetu kuhakikisha kwamba hafanyi vitendo vya kuhatarisha amani, kuharibu mali za watu na kutishia maisha ya watu ambao hawana hatia. Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya 1984, lengo kubwa la Serikali ni usalama na hali nzuri kwa wananchi, kama ilivyobainishwa katika kifungu 9(2)(b).

Kwa hivyo, Serikali itafanya kila jitihada kuhakikisha kuwa wananchi wote wanakuwa salama. Aidha, wale wote watakaobainika kushiriki katika vitendo vya hujuma na kuhatarisha amani waelewe kwamba sheria itafuata mkondo wake bila ya kumuonea au kumdhulumu mtu ye yote.

Viongozi wa siasa ni wajibu wetu tufanye siasa kwa kuzingatia misingi ya sheria, Katiba ya nchi yetu na kufuata katiba na maadili ya vyama vyetu. Ni jukumu letu wanasiasa tushindane bila ya kudharauliana na kugombana. Wanasiasa ni vyema tukakumbushana kwamba sote ni wamoja tunatafautiana kwa vyama vyetu na tunaweza kushindana bila ya kuhasimiana na kukejeliana. Lengo la kuanzishwa vyama vingi ni kushindana kwa sera na kuchochea maendeleo.

### **Ndugu Wananchi,**

Wakati tuna furaha ya kusherehea Sikukuu, ni muhimu tukakumbushana kwamba bado maradhi ya kipindupindu yapo; ingawa kutokana na juhudhi za Serikali yetu na wananchi tumeweza kwa kiasi kikubwa kuzuulia maambukizo katika sehemu zote za Unguja na Pemba. Kwa

hivyo, tunahitaji kuendeleza ushirikiano na juhudi zetu ili tuendelee kuyadhibiti maradhi hayo.

Ni wajibu wetu tuendelee kuyafuata masharti yaliyowekwa na Wizara ya Afya, Mabaraza ya Manispaa, Halmashauri pamoja na kupokea miongozo na inayotolewa na wataalamu wa afya. Kadhalika, tuhakikishe kuwa tunasherehekea Sikukuu katika maeneo yaliyotengwa na Manispaa na Halmashauri zetu. Wazazi tunatakiwa tuwe makini kuwapa watoto wetu miongozo ya kiafya na tuwakataze wasile vyakula vinavyoweza kusababisha maambukizo ya kipindupindu. Serikali inaendelea kufanya tathmini ya maradhi haya na itatoa taarifa kadri hali itakavyoendelea. Natoa wito kwa wananchi waendelee kufuata masharti na kanuni za afya na watimize usafi ili tuepukane na maradhi hayo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azipe baraka juhudi zetu na atuwezeshe kuyatokomeza maradhi hayo ili hatimae tuweze kuendeleza maisha yetu katika hali ya kawaida.

### **Ndugu Wananchi,**

Serikali imechukua juhudi kubwa katika kuwaelimisha wananchi juu ya athari za vitendo viovu kwa kushirikiana na wanasiasa na viongozi wa dini. Kwa bahati mbaya, bado tunaendelea kupata taarifa ya kuwepo kwa vitendo vya unyanyasaji na udhalilishaji wa kijinsia wanavyofanyiwa wanawake na watoto katika jamii yetu. Jambo baya zaidi na la kusikitisha kwamba baadhi ya vitendo vilifanywa katika mwezi Mtukufu wa Radhamani, tena mchana, Mwenyezi Mungu atuepusha na atuhifadhi na balaa hili. Sote tunapaswa tuwakemee na tupambane nao wanaofanya vitendo hivi. Pale panapotakiwa utolewe ushahidi, basi

wananchi wanaohusika wajitokeze kutoa ushahidi; kwa kufanya hivyo watafanya wajibu wao kwa ajili ya kuwalinda watoto wetu. Vitendo hivyo ni kinyume na mafundisho ya dini, ni kinyume cha utamaduni na malezi yetu na vile vile ni kinyume na haki za binadamu na mikataba ya Kitaifa na Kimataifa.

Katika kipindi cha mwaka mmoja na nusu uliopita, Serikali ilianza kuchukua hatua. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na tatizo hili ni kuanzisha kampeni ya kupiga vita vitendo vya udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto kwa kushirikiana na washirika mbali mbali. Serikali ilitoa elimu ya masuala ya udhalilishaji wa kijinsia kupitia semina, makongamano na vyombo vya habari pamoja na kuwahamasisha wananchi kutoa taarifa za vitendo hivi. Kadhalika, Serikali iliifanya marekebisho Sheria ya Mtoto Namba 6 ya mwaka 2011 ya kumlinda mtoto. Vile vile mahakama ya watoto nchini ilianzishwa pamoja na kuongeza idadi ya vituo vya mkono kwa mkono hadi kufikia 6. Kadhalika vituo hivi vilipatiwa nyenzo na watendaji ili kurahisisha shughuli zake za kuwahudumia wale walioathiriwa na vitendo vya udhalilishaji.

### **Ndugu Wananchi,**

Pamoja na jitihada hizo, bado juhudini za pamoja zinahitajika katika kuhakikisha kuwa tunakabiliana kwa ufanisi na vitendo vya udhalilishaji na unyanyasaji wa kijinsia. Idadi ya vitendo vya aina hii inayoripotiwa, inathibitisha ukubwa wa tatizo liliopo, mbali na vile vitendo ambavyo taarifa zake hazifikishwi katika taasisi zinazohusika.

Kwa mujibu wa hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto iliyowasilishwa katika Baraza la Wawakilishi hivi karibuni, imebainika kuwa bado kuna idadi kubwa ya malalamiko yaliyowasilishwa katika Wizara hiyo kuhusu vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto. Imeelezwa kuwa jumla ya malalamiko 100 (46 Unguja na 54 Pemba) yanayohusu vitendo vya aina hiyo yameripotiwa. Aidha, taarifa iliyokusanywa katika vituo vyote 6 vya mkono kwa mkono Unguja na Pemba inaonesha kati ya Julai, 2015 hadi Aprili, 2016 kumeripotiwa matukio 875 Unguja na 139 Pemba ya udhalilishaji wa watoto.

Wanaofanya vitendo hivi ni watu ambao hawana huruma na ni makatili. Katika kulifafanua suala la huruma kwa watoto, Mtume Muhammad (S.A.W) ametueleza kwamba: "*Kuwalinda watoto ni huruma, na huruma ni kinga*". Kadhalika, Mtume Muhammad (S.A.W) amesema "*Si katika sisi yule mtu asiyemhurumia mdogo na asiyejua haki ya mkubwa (asiye mheshimu)*". Aidha, Mtume Muhammad (SAW) Ametueleza tena: "*Rehemuni (sikitikieni) wenzenu, nanyi mtarehemewa.*"

Hadithi zote hizi zina mazingatio makubwa na muhimu katika jitihada zetu za kulea watoto wetu na kupiga vita vitendo vya kikatili na unyanyasaji wa kijinsia katika jamii yetu.

Ilivyokuwa tumebakisha miezi sita, ili kukamilisha miaka 2 tuliojipangia kufanya kampeni dhidi ya udhalilishaji wa wanawake na watoto tunapaswa tulitafakari na kulifanyia kazi upya suala hili. Hili ni jambo kubwa na lazima tuendelee kupambana nalo hadi tufanikiwe. Nasaha

zangu kwa vyombo vyanya sheria ni kutoa ushirikiano kwa wananchi wanaofikwa na tatizo hili. Vile vile, wananchi waendelee kutoa taarifa katika vyombo vinavyohusika ili wahusika wakithibitika, waweze kuchukuliwa hatua za kisheria. Kadhalika, kwa upande wa walimu, masheikh na viongozi wote wa madhehebu ya dini nao waendelee kuielimisha jamii juu ya ubaya wa vitendo hivi ili tupate jamii ya wacha Mungu.

### **Ndugu Wananchi,**

Tukiwa katika siku ya mwanzo ya sikukuu ya Idd el Fitr, natumia fursa hii kutoa shukurani kwa wafanya biashara wote walioitikia wito wa Serikali wa kutopandisha bei ya bidhaa zilizohitajika zaidi katika kipindi cha mwezi wa Ramadhani. Waelewe kuwa kitendo hicho cha imani ni ishara njema ya utii wa sheria, kinaongeza baraka katika biashara na kinafadhila kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu awajaalie kila la kheri katika shughuli zao.

Kadhalika, naipongeza Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira pamoja na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kwa kuwapatia maji safi na salama wananchi ambao walikua na uhaba wa maji safi na salama katika maeneo yao. Vile vile, shukurani zangu nazitoa kwa Jeshi la Polisi na Vikosi vyote vyanya Ulinzi na Usalama, kwa kuimariswa ulinzi katika kipindi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani, ambapo wananchi waliweza kutekeleza ibada zao katika hali ya amani na utulivu. Bila ya shaka, Jeshi la Polisi na Vikosi vyetu vyanya Ulinzi na Usalama vitaendelea na hatua hiyo katika kipindi hiki cha sikukuu, ili wananchi na wageni

waliopo waweze kuifurahia sikukuu na kufanya shughuli zao kwa usalama.

### **Ndugu Wananchi,**

Natoa shukurani na pongezi maalum kwa ndugu zetu ambao si waislamu, kwa ushirikiano waliota kwa ndugu zao waliokuwa katika funga, kwa uvumilivu wao katika kujizuwia kufanya mambo ambayo yangeleta karaha kwa ndugu zao waislamu, lakini walijizuwia kwa kuuhestimu Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Hii ni ishara njema ya kukomaa kwetu katika kustahamiliana na ustaarabu uliojengwa katika nchi yetu tangu kale na dahari na tuna wajibu wa kuuendeleza.

Kwa kufahamu kwamba tayari wapo waislamu wenzetu wanaojiandaa kwenda kuitekeleza ibada ya Hijja mwaka huu, natumia fursa hii kuwatachia matayarisho mema. Tumuombe Mwenyezi Mungu awajaalie kwenda kuitekeleza ibada hiyo kwa salama. Inshaalla Mwenyezi Mungu azikubali ibada zao zote watakazozifanya na awarudishe nyumbani kwa salama.

Kabla sijamaliza hotuba yangu, natoa shukurani maalum kwa Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi Dk. Abdulhamid Yahya Mzee na Wasaidizi wake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango; Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa muda mfupi, baada ya kuwapa maelekezo ya kuufanya matengenezo ukumbi huu na maeneo mengine. Vile vile, naupongeza uongozi wa

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa kazi walioifanya ya kutia lami mbele ya jengo hili, Kadhalika, natoa pongezi kwa Idara Maalum za SMZ (KMKM na Chuo cha Mafunzo), kwa kukamilisha kwa umahiri mkubwa kazi mbali mbali za kiufundi walizopewa wakati wa matengenezo. Ukumbi unapendeza sana. Tumepata ukumbi huu mzuri wakati ambapo Ukumbi wa Salama wa Hoteli ya Bwawani kwa sasa hautumiki kwa shughuli kama hizi. Hata hivyo, ni jukumu letu tuutunze ukumbi wetu huu tukizingatia ule msemo maarufu usemao kitunze kidumu.

Mwisho, namuomba Mwenyezi Mungu aijaalie nchi yetu kila la kheri. Atupe maisha mema duniani na akhera. Atulinde na maovu na uadui. Atujaalie tuwe watu wema, wenye umoja na mshikamano. Awape uzima wagonjwa wetu na awarehemu wazee wetu, ndugu, jamaa na wote waliokwishatangulia mbele ya haki. Natoa shukurani kwenu nyote mliohuduria katika Baraza hili na wale wanaolifua tilia kupitia vyombo vya habari. Namuomba Mwenyezi Mungu aturudishe sote majumbani mwetu kwa salama na amani.

### **IDD MUBARAK**

### **WAKULLU AAM WA ANTUM BIKHEIR**

**Ahsanteni kwa kunisikiliza.**